



**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 1**  
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**  
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Monday 19 May 2003 (morning)

Lundi 19 mai 2003 (matin)

Lunes 19 de mayo de 2003 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Rédiger un commentaire sur un seul des passages.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento.

*Kifafanue kimoja kati ya vifungu vifwatavyo:*

**1. (a)**

	Kiumbe uzito wake Ilivyo ueleweke Ni vile vitendo vyake Ulipo uzito wake	siwo wa vyuma na mawe huo uzito wenyewe visivyo na mfanowe si ye ye vyake vitendo
5	Vizito vyake vitendo Vikubwa vyake vishindo Kwake iwe huna fundo Ulipo uzito wake	asiyejuwa ajuwe hilo tulipambanuwe kuwa achukiwe nawe si ye ye vyake vitendo
10	Yenye kheri na kipato Halitomwishia joto Huwa katika majuto Ulipo uzito wake	pindi atekelezewe na moyo wake utuwe na kulaumu wenziwe si ye ye vyake vitendo
15	Hata ukimwokowa Hatoshukuru kwa kuwa Fadhila huzipinduwa Ulipo uzito wake	penye janga umvuwe na kukuona mwenzive kukuangamiza wewe si ye ye vyake vitendo

Kutoka *Kimbunga* na Haji Gora Haji (1994)

1. (b)

Nuksani, mfalme mpya, alikuwa ni mtu mwenye choyo sana; kwa hivyo ufalme tu haukumtosha, alikuwa macho yake kawakodolea raia. Akimwona raia katononoka kidogo kwa maisha akimnyang'anya. Alikuwa akiamini kuwa hakuna mtu yeoyote anayefaa kustarehe, hakuna anayefaa kula na kuva, ila mfalme. Kwa hivyo alizungusha 5 nyavu zake kila sehemu inayoweza kupatikana riziki na kuikamata yeye. Mfalme Nuksani akaanza kuleta utawala wa kinguvu kwa raia zake.

Raia walikuwa hawawezi hata kutoa pumzi, na kwa muda mfupi wa utawala wa Mfalme Nuksani nchi nzima ikaanza kuingia fujo na zogo. Raia wakaanza kutawanyika, 10 wa mjini wakakimbilia mashamba na wa mashamba wakakimbilia mjini. Mke alikuwa hamjui mume, baba hamjui mwana na mwana hakumjua mzee. Ikawa chombo msagurano, raia hawatambuani. Mambo yakaanza kubadilika kwa haraka nchini humo. Tamaa za majumba zikaanza kukatika. Neema iliyokuwemo katika nchi ikaanza 15 kutoweka kidogo kidogo, kwa sababu choyo na husuda sivyo vinavyojenga nchi. Mfalme Nuksani, licha ya kujenga na kuendeleza mbele miji, bali hata kutengeneza yaliyokwisha jengwa na Mfalme Ihisani alishindwa. Punde si punde baadhi ya majengo ya nchi hiyo yakaanza kuporomoka na kubakia viwanja. Wafanya biashara, ambao destruri siku zote wanafuata maendeleo, wakaanza kutoweka. Nchi ikadamirika. Aaa! Hawakukosa waliosema, "Pavumapo Palilie, si kazi kudamirika".

Kutoka *Pavumapo Palilie* na F H Nassor (1972)

---